


# KIJASHO CHEMBAMBA

Na: Richard MWAMBE

©Jamvi la Simulizi 2025

# SURA YA 1

## ANTANANARIVO
## Madagaska

VUA ya rasharasha ililifanya Jiji la Antananarivo kuwa Mchepechepe. Tope jepesi lilizijaza barabara zisizo na lami zilizokatisha kwenye viunga vyake. Hoteli ndogo ya Le Combava yenye hadhi ya nyota tatu ndiyo iliyomhifadhi Kamanda Amata kwa takribani saa 48 tangu awasili katika jiji hilo. Mara hii hakuja kustarehe na warembo wa Kimalagash bali alikuja kazini. Kazi iliyohitaji umakini na akili ya kiwango cha juu kuliko unavyofikiria. Hata yeye mwenyewe alilijua hilo na ndiyo maana hakutaka kabisa kupoteza hata nukta ya utimamu wake kwa mambo aliyoyaita kwa siku hiyo 'yasiyo na maana'.

Mchana huu alikuwa na kazi moja tu, kazi aliyopewa na bosi wake, Madam S. Kuhakikisha anaipata 'Kokwa'. Mpaka sekunde hiyo tafutishi zao zilionesha wazi kuwa Kokwa hiyo ipo Antananarivo na huko haitakaa muda mrefu kwani inapaswa kupelekwa pahala pengine. Hilo halikutakiwa kufanikiwa hata kidogo. Alipohakikisha amekamilika, alikuwa tayari kuingia mjini kukabiliana na

adui yake. Kila kitu alishakiweka sawa. Kilichomsubiri ni utekelezaji tu. Akiwa ndani ya suti safi nyeusi, iliyotanguliwa na shati jeupe na tai ndefu nyeusi, alikuwa tayari kwa safari. Kofia nyeusi ya Kiyahudi akaipachika kichwani pake huku mkononi akiwa na fimbo ya mpingo iliyokuwa na nakshi nzuri za kupendeza.

Akatoka nje ya chumba chake na kuelekea mapokezi. Pale akaacha kadi ya chumba na kufuata maegesho ya hoteli hiyo. Aliliendea gari lake alilokodi kwa shughuli za hapo, Renault la kisasa kabisa lilikuwa likimsubiri. Akaingia na kutulia nyuma ya usukani. Katika nchi ya Madagaska, magari aina ya Renault na Citroen ni maarufu sana hivo na yeye akakodi moja ya aina hiyo. Kukodi gari hilo aina ya Renault hakukuwa kwa bahati mbaya bali ni moja ya kufanya kazi zake kuwa rahisi zaidi awamo jijini humo. Akatia funguo na kuipa moto injini, kisha taratibu akayaacha maegesho na kuelekea kule anakokutaka.

Alikuwa makini barabarani kwani kuna kitu ambacho alikigundua siku hiyo. Hii ilikuwa siku yenye nyendo za tofauti kabisa kwa wakazi wa jiji hilo. Kwanza aliwaona wawili wawili, yaani kila alipo mwanaume palikuwa na mwanamke. Mavazi waliyokuwa wamevaa yalimwachia mswali mengi kiasi. Yalikuwa ya kitamaduni zaidi. *Kuna nini leo?* Akajiuliza. Lakini kwakuwa hilo halikuwa la msingi katika kazi yake, hakulititilia maanani. Akilini mwake alijaa mtu mmoja tu, Mikhail Planchikov. Huyu ndiye

haswa aliyemfanya kijana huyu kufika Antananarivo. Kila kitu kilikuwa sawa, na sasa alikuwa anaelekea pahala alipo bwana huyo, Mzungu kutoka Russia, mtaalamu wa masuala ya nyuklia, aliyekuwa Tanzania kwa utafiti wa madini hadimu ya urani miaka takribani mitano iliyopita.

Le Louvre Hotel ndiyo haswa alipokuwa anahitaji kufika. Kwa mwendo wa taratibu, aliendesha katika Barabara ya Chinoise Saissoniere. Lakini, jambo hasilolitegemea alikutana nalo. Kizuizi cha askari wa usalama barabarani kuelekea Boulevard de L'Europe, barabara iliyokuwa sahihi sana kwake kufika pale anapotaka. Mmoja wa wale askari akalisogelea gari la Kamanda Amata pale liliposimama. Ilikuwa ni mita chache sana kutoka kwenye kile kizuizi.

"Samahani, unaelekea wapi?" yule askari kijana akamuuliza Amata baada ya kioo kushushwa.

"Le Louvre Hotel…" Amata akajibu kwa Kifaransa cha kubabaisha.

"Le Louvre Hotel… ok! Sasa itabidi ubadili njia, tumia Boulevard de L'Europe kuelekea Cathestudio… huko utapata maelekezo mengine," yule kijana akamuelekeza.

"Kuna nini mpaka mfunge barabara?" akauliza.

"Leo ni kilele cha sherehe ya Canival, hivo watu wengi watakuwa kwenye hii barabara usiku huu wakisherehekea," yule askari akajibu na kumwacha Amata huku akielekea upande mwingine kusaidia wengine. Amata akageuza gari

lake na kuchukua barabara ile aliyoelekezwa. Ilimchukua dakika kama ishirini na tano hivi kufika eneo analolitaka. Lakini isivyo bahati barabara nyingi zilikuwa zimefungwa kwa hivo ikampasa kuegesha gari pahala pengine.

Akatereka na kujiweka vizuri, kisha akavuta hatua kuelekea upande ambako kelele nyingi za muziki na ngoma zilisikika. Baada ya kupenya hapa na pale, akatokea kwenye hiyo barabara kubwa na kukuta umati wa watu. Mtaa wote ulirindima kwa muziki, ngoma, vinywaji, vyakula na burudani za kila aina. Pamoja na kuwa hapo Antatanarivo kwa siku mbili hakujua kabisa kama siku hii kutakuwa na sherehe hizi kubwa. Akatuliza akili kwanza. Akatia mkono mfukoni na kutoka na karatasi ndogo mkononi mwake.

*'Le Louvre Hotel*
*7:15PM'*

Alipokisoma, akaitazama saa yake kisha akakirudisha mfukoni. Akainua macho yake na kuiona hotel ile upande wa pili wa barabara. Hivo ilimpasa kuvuka mpaka upande ule na wakati huo umati wa watu ulikuwa umehanikiza barabara yote yaani upande huu na ule kule. Moyo wake ulimwenda mbio maana ni muda mrefu sana hajakutana na kashkash za namna hii. Damu ilipoa. Ilikuwa saa moja na dakika tano usiku alipojitoa pale aliposimama na kujichanganya katikati ya burudani. Lengo haikuwa

kuburudika bali kuvuka kuelekea upande wa pili. Akiwa katikati ya umati ule, alihisi mkono wake ukishikwa na mwingine. Kabla akili yake haijatenda vinginevyo, hisia za mwili wake zilimtuliza. Ulikuwa mkono laini sana ambao mtekenyo wake ulipenya mpaka kwenye chini ya mwili wake. Akageuka na kumtazama huyo aliyemshika. Alikuwa kiumbe mrembo wa kike, macho yake kama binti wa Farao yalimfanya awe mithili ya Cleo Patra. Kiblauzi alichovaa mwilini mwake kilikuwa chepesi lakini kilichoshikamana na mwili wake kiasi kwamba kilifanya matiti mawili ya duara yakae katika mwonekano wa kuvutia. Alikuwa kadiri ya miaka ishirini na tano hadi thelathini hivi.

"Endelea kwenda…" sauti nyembamba na nyororo ya mwanamke yule iliyapenya masikio ya Amata. Akatii. Walipomaliza kuvuka ule umati wa watu na kutokea upande wa pili, yule mwanamke akaongeza mwendo na kumfanya Amata naye afanye vivyo hivyo. Wakalielekea moja ya jengo kubwa lililo jirani na ile hoteli. Mbele tu jengo hilo, yule mwanamke akasimama mbele ya Amata na kumpiga busu la kinywani. "Ina maana warembo hutuoni au? Leo ni siku yetu ya kufurahia maisha na wageni, name nimekuwahi, mwanaume wangu wa leo!" akasema kwa sauti ya kumtoa nyoka pangoni. Kamanda Amata akamtazama upande wa nyuma. Mh! Si mbaya. Kijisketi alichovaa kiliyaacha nje mapaja manene na manono. Kabla hajasema lolote, akavutwa ndani ya lile jengo. Akaingizwa

kwenye kambarau na kupelekwa mpaka ghorofa ya tatu. Amata alikuwa kama kondoo anayepelekwa machinjioni. Kimya, mkukumkuku, anaenda tu.

Katika korido ndefu ya sakafu hiyo ya tatu, aliona wanawake wengi na vijana wa kiume katika mikao ya kimahaba. Hapakuhitaji 'D2' kujua kuwa pale palikuwa dangulo. Mlango namba 35 ndipo yule mwanamke akachomeka funguo na kuufungua mlango. Wakaingia ndani na mlango ule ukafungwa. Ndani hapo palikuwa sebule kubwa na nzuri yenya maua kadha wa kadha. Zuria jekundu lilitandikwa kila pahala kisi kwamba hapakua na hata kipande cha sakafu kilichoonekana.

"Njoo!" yule mwanamke akasema huku akiufungua mlango mwingine. Amata akaingia na kukaribishwa na chumba kikubwa chenye kitanda kikubwa, kizuri, chenye nakshi za kila namna. Manukato ya gharama na kila kitu ambacho kingewasukuma wapendanao kuashiriki tendo, kilikuwamo. Yule mwanamke akatupa kipochi chake kitandani, naye akajitupa na kuketi. Upande alioelekeza mgongo palikuwa na dirisha kubwa sana, mapazia yake mawili yalikuwa upande huu na ule na kuacha kioo tu kiasi kwamba aliweza kuona mpaka hoteli ile ya Le Louvre.

"Wewe ni nani?" Amata akafungua kinywa chake kwa mara ya kwanza.

"Usihofu, upo kwenye mikono salama Amata!" yule mwanamke akajibu. Jambo lililokuwa likimshangaza Amata

ni lugha. Mwanamke yule alikuwa akiongea Kiswahili safi kisicho na mikwaruzo. Lafudhi halisi kabisa ya Kitanzania. "Kukuleta hapa nimefanya makosa makubwa sana…" akasema. "Makosa ambayo yatagharimu uhai wangu… hata hivyo ni kwa ajili yako," akaongea kwa sauti ya chini lakini ilikuwa 'stereo' kwelikweli.

"Wewe ni nani?" Amata akarudia swali, "Na kwanini uweke maisha yako reheni kwa ajili yangu?" akaongeza swali. Akatazama saa yake, ilitimu saa moja na dakika kumi na mbili jioni. *Bado dakika tatu windo langu lifike!* Akawaza. Akarudisha macho kwa yule mwanamke.

"Naitwa Afrika!" yule mwanamke akajibu.

"Afrika?" Amata akauliza ili kupata uhakika.

"Ndiyo, najua itakushangaza, ila jina langu ni Afrika…" akajibu tena. Amata akaona mwanamke yule anampotezea muda. *Ametumwa!* Akawaza. *Uwepo wangu ushajulikana hapa, sasa nione la kufanya kwa muda!* Akajiambia moyoni mwake.

"Asante Afrika, kwaheri… sipo kwa huduma unayotaka kunipa. Ila nikimaliza kazi yangu nitakutafuta unihudumie," Amata akasema huku akianza kuuelekea mlango.

"Sivyo Amata! Hivi we ni mpelelezi gani ambaye hata ushangai nalijua jina lako kwa ufasaha namna hii?" Afrika akauliza.

“Kwa kazi yangu, kila mtu analijua jina langu, tena analijua zaidi ya mimi ninavyolijua… sishangai!” ASmata akasjibu na kushika kitasa.

“Sikiliza Amata! Wanajua kama upo Antatanarivo, wanajua nyendo zako zote, wanajua kama saa hii utakuwa eneo hili, wanajua kama unamtaka Mikhail Planchkov, wanajua kuwa umetumwa kuitafuta ‘kokwa’…” Afrika alizungumza huku macho yake yakiwa yamejawa machozi. Amata aliondoa mkono kwenye kile kitasa na kusimama kidete. Akashusha pumzi na kumwangalia Afrika pale alipoketi. Afrika aliinua mkono wake na kuuelekeza kichwani pake ili kutoa ua alilojipamba. Macho ya Amata yalikuwa yakiufuata mkono huo na yalipotua, moja kwa moja yalikuwa yakitazama dirisha lile kubwa. Lahaula! Macho yake yalijikuta yakitazamana na bomba la bunduki ya kirussia likimtazama. Kwa harakaharaka aliijua bunduki hiyo, IZMASH Saiga12 gauge. Akili ya haraka ikamjia. *Tunashambuliwa!* Akawaza na kujirusha upande wa pili. Kioo cha lile dirisha kikatawanyika vipande vipande na kuleta tafrani ndani ya kile chumba. Risasi zile tatu zilizomkoa Amata ziliishia ukutani. Akachomoa bastola yake na kusimama nyuma ya pazia akitupa jicho huku na huko. Amata akawahi kwenye dirisha jingine na kuvuta pazia kuangalia nje. Aliona vijana wawili wa Kiafrika wakitoka kwa kukimbia kwenye ile hoteli. Vijana wale

walikuwa wakielekea kwenye jengo lilelile alilokuwamo yeye na Afrika.

Kisha Mzungu mmoja mtu mzima akatoka kwenye mlango mkubwa wa ileile hoteli akisindikizwa na watu wegine wawili wakaingia kwenye gari na kuondoka kwa kasi. Amata akashusha paumzi na kuuelekea ule mlango. Akafungua na kuuacha wazi kidogo. Haikupita dakika akahisi mlango mkubwa wa sebuleni ukifunguliwa. Muda wote huo, Afrika alikuwa sakafuni kimya. Damu kidogo ilionekana kwenye kifua chake. Amata akatulia palepale ili kuona kitachojiri. Hakukosea, domo la IZMASH Saigalikatangulia huku likiusukuma mlango taratibu. Amata akatulia kimya na kusubiri sekunde kadhaa alizozitaka.

Yule bwana akaonekana kusimama mlangoni, maana domo la ile bunduki halikusogea kuingia ndani. Kwa kasi ya ajabu, Amata alkamata ule mtututu wa IZMASH Saiga na kuvuta ndani. Yule jamaa akajikuta kaingia pasi na kutarajia. Pigo moja lililopigwa kwa umahiri lilitua nyuma ya shingo ya huyo bwana. Akapepesuka na kuvuta hatua za kiwewe mbele. Kabla hajatulia alijikuta anapigwa kabali ya shingo na kuvutwa chini. Akabwagika kama gunia la mpunga. Risasi moja ikadididimia mwilini mwake. Amata alipomnasua kwenye ile kabali, yule jamaa alitepeta.

“Wewe ni nani?” akamuuliza. Yule bwana alikuwa akivuta pumzi zake za mwisho-mwisho. Hakujibu, aligeuza sura na kumwangalia Amata huku povu likimtoka

kinywani. Kwa haraka Amata akampekuwa kijana yule. Akachukua kitambulisho chake, leseni ya kuendeshea gari, simu ya mkononi. Kishindo cha mlango kupigwa kwa nguvu kikamgutusha pale chini. Kamanda Amata aliruka sarakasi na kutoka kwenye lile dirisha kubwa mpaka nje ambapo alianguakia juu ya jengo fupi jingine. Risasi kadhaa zilimkosa. Maumivu ya mgongo yalimtambaa mwili mzima lakini hakuwa na muda wa kuyatii. Alivingirika na kujirusha chini ambapo alitua juu ya vyakula vilivyokuwa vikiuzwa hapo barabarani. Alichijua ni kunyanyuka na kutimua mbio kutafuta usalama wake huku watu wakipiga kelele za kumshangilia wasijue nini kimetukia.

✠✠✠

Kamanda Amata aliegesha gari lake nje ya hoteli ya Le Combava. Akateremka na kuelekea chumbani kwake. Alipoufikia mlango akasimama kwanza kabla ya kufanya lolote. Akatazama baadhi ya alama zake alizoweka na kuzikuta zipo salama kabisa. *Hawajaja!* Akajiambia na kupachika kadi ya kufungulia mlango. Ni kwa kupachika kadi hii tu ndipo utaruhusu kila kitu kifanye kazi ndani ya chumba hicho. Alitoa kila kitu alichohukua kwa yule jamaa na kubwaga kitandani. Akaliendea begi lake na kutoa vidonge kadhaa akameza ili mwili wake utulie dhidi ya maumivu makali. Akavua nguo zote na kujinyoosha

kidogo. Alipoona mwili upo sawa kwa kiwango fulani akaliendea bafu ili ajimwagie maji. Alipopiga tu hatua kuingia bafuni humo, almanusura aanguke. Alichokiona kwenye beseni kubwa la kuogea hakikuwa kitu cha kawaida.

Mwili mbichi wa Afrika ulikuwa umelazwa ndani yake huku shingo ikining'inia upande wa pili na kuacha koromeo linalovuja damu nzito. Amata alihisi kama kapigwa shoku ya umeme, aliganda akiwa katoa macho. *Wamemleta saa ngapi hapa?* Akajiuliza. Alipopiga hesabu zake tangu yeye atoke kwenye lile jengo na kumwacha Afrika pale chini mpaka kufika hapo hotelini hakuna kasi ya kibinadamu inayoweza kufanikisha jambo hilo. Akatulia lakini jicho lake bado lilikuwa likiutazama ule mwili. Mbisho wa hodi ukasikika kutoka mlangoni. Akashusha pumzi na kuliacha lile bafu. Haraka haraka akavaa suruali yake na shati. Akauendea mlango na kuufungua. Mbele yake walisimama askari wawili waliovalia nadhifu kabisa pamoja na kijana mmoja aliyevalia sare za wafanyakazi wa hoteli ile.

"Tumepata taarifa kuwa kwenye chumba hiki kumesikika kelele za mwanamke anayeomba msaada.. tunataka kupekua," mmoja wale askari akaeleza. Amata akamtazama yule mfanyakazi aliyekuja na hao askari na kuona kabisa hayuko sawa, wasiwasi na woga vilimtawala.

“Hizo kelele mmesikia saa ngapi?” akawauliza huku akimalizia kufunga vishikizo vya shati lake.

“Hayo siyo maswali ya kuuliza,” akajibu yule askari na kumsukumia ndani Amata. Moja kwa moja akauendea mlango wa bafu. Wakati huo, Amata keshachukua vilevikolokolo pale kitandani na kutia kwenye koti lake. Yule askari akamwita mwenzake na yule mfanyakazi ili washuhudie kilichotokea kule bafuni. Kama walikuwa hawajui, basi Amata alisubiri nukta hiyo tu. Alivuta mkoba wake na kutoka. Kabla hajaufunga mlango akatupa chini kichupa kidogo ambacho kwa kupasuka kwake kilitoa moshi mzito. Akafunga mlango na kuchomoa kadi mlangoni.

“Endeleeni na uchunguzi wenu… mnacheza michezo ya kitoto mbele yangu…” akasema huku akiondoka eneo hilo. Akaingia kwenye gari lake na kuyaacha maegesho ya ile hoteli. Akatokomea mjini. Breki yake ya kwanza ilikuwa katika Kliniki ya Masista wa Franciscaine Ankadifotsy. Hakuwa na lolote hapo zaidi ya kuegesha gari na kuliteleKeza….

USIKOSE mwendelezo wa hadithi hii hapahapa ‘kitabumarket’ kila JUMAMOSI na JUMATANO.

TAFADHALI tuachie comment yako kupitia **Whatsapp 0766974865**